

# MUONGOZO WA UOMBAJI WA UFADHILI WA COMMONWEALTH MASTER'S SCHOLARSHIPS



COMMONWEALTH SCHOLARSHIP  
MASTERS APPLICATION 2025

## **Umetayarishwa na:**

Mnufaika wa Ufadhili wa Commonwealth (Commonwealth Master's Scholar-2024)

Mchaguliwa wa Ufadhili wa China (Selected candidate for CSC type A-Masters, 2024)

## **TANBIHI:**

Maoni yaliyotolewa katika muongozo huu yanatokana na uzoefu wa mwandishi ambae ni mnufaika wa Ufadhili huu. Maoni haya hayatokani na Kamisheni ya ufadhili wa Commonwealth (CSC) au Ofisi ya Maendeleo, mambo ya nje na Jumuiya ya madola (FCDO).

**Ruhusa ya kusambaza kwa kila anayehitaji imetolewa**

## YALIYOMO

UTANGULIZI WA MWANDISHI.....	3
MAELEZO JUU YA UFADHILI WA COMMONWEALTH MASTER'S SCHOLARSHIPS.....	6
VIGEZO STAHIKI VYA UFADHILI HUU (ELIGIBILITY CRITERIA).....	10
NYARAKA ZINAZOHITAJIKA.....	10
UCHAGUZI VIGEZO VYA UCHAGUZI (CSC SELECTION PROCESS AND CRITERIA).....	11
HATUA ZA KUFANYA ILI KUOMBA UFADHILI HUU.....	13
JE NI LAZIMA UWE NA CHETI AU UFANYE MTIHANI WA KIMATAIFA WA KIINGEREZA (IELTS AU TOEFL)? .....	17
NAMNA YA KUJIBU INSHA 4 ZA CHEVENING NA MIFANO.....	18
NAMNA YA UOMBAJI HATUA KWA HATUA.....	20
KUHUSU REFEREES.....	22
NAMNA YA KUOMBA VYUO VYA UINGEREZA.....	23
KUHUSU DEPOSIT.....	28
NAMNA YA KUANDIKA EMAIL (Professional email) .....	28
VIPINDI VYA GOOGLE MEETING.....	29
KWA NINI NIMEANDIKA MUONGOZO HUU?.....	30
MIONGOZO MENGINE .....	31

## UTANGULIZI WA MWANDISHI.

Ndugu watanzania wenzangu, tafadhali naomba mfahamu mambo kadhaa hasa katika kuomba ufadhili.

1. Kila ufadhili una vigezo vyake, hivyo unapaswa kujikita kwenye vigezo. Kuna baadhi ya ufadhili unaomba peke yake na chuo unaomba peke yake mfano Chevening, Commonwealth, Chinese Scholarship na kuna ufadhili unaomba na vyuo kwa pamoja katika ombi moja mfano Turkish Buslari scholarship, KNB Indonesian Scholarship na nyenginezo. Pia baadhi ya vigezo huwemo katika ufadhili Fulani na hukosekana kigezo hicho katika ufadhili fulani, mfano kigezo cha umri au uthibitisho wa ufasaha wa lugha ya kiingereza. Hivyo kabla ya kuanza maombi ya ufadhili au chuo husika, tafadhali pitia na soma maelekezo yote, hii itakusaidia kuwa na uhakika wa unachokifanya na kukuongezea nafasi ya kufanikiwa katika maombi yako.
2. Fadhili na vyuo vyingi duniani vinavyopokea wanafunzi wa kimataifa (International students) huweka maelekezo juu ya namna ya kuomba, au huweka majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara (Frequently Asked Questions-FAQs) au huweka mawasiliano yao iwapo utahitaji kuwasiliana nao. Tafadhali hakikisha unasoma maelekezo haya au unapitia FAQs, na ikibidi fanya mawasiliano nao iwapo utakwama au utapata changamoto yoyote.
3. Tafadhali fahamu kuwa fadhili nyingi huwa na ushindani wa hali ya juu, hivyo hakikisha unakidhi vigezo husika lakini pia unafata maelekezo husika kabla hujaanza kufanya maombi husika. Kusoma maelekezo husika kutakusaidia kutambua nini unafanya na hii itakupunguzia maswali au sintofahamu inayojitokeza wakati unafanya maombi yako.
4. Kufanya maombi ya Fadhili hata kama ni za kulipiwa kila kitu (Fully funded) mara nyingi huhusisha gharama kama vile muda na pesa. Mfano unaweza kutumia pesa katika kutoa nakala, kuthibitisha nakala zako kwa mwanasheria, kubadilisha nyaraka ngumu kuwa nyaraka laini (scanning), kuperuzi mtandao na mambo mengine. Unapaswa kutenga masaa kadhaa kila siku kupitia taarifa za scholarship na kuangalia kama una sifa.
5. **JIAMINI**, kama wengine walipata ufadhili, hata na wewe unao uwezo wa kupata. Muhimu ni **KUJITUMA** na kufuata maelekezo yote yanayotakiwa. Tafadhali pitia mfano wa uandishi wa email ambao nimeuainisha katika muongozo huu ili utumie kama njia ya mawasiliano iwapo utahitaji kufanya hivyo. Kumbuka kuwa mawasiliano kwa njia ya email ndio njia kuu ya mawasiliano kwa fadhili au vyuo vya nje ya nchi.

6. Usisahau kumtambuliza Mwenyezi Mungu kwenye kila kitu ufanyacho. Kwa hakika haswa utakutana na changamoto kadhaa, tafadhali usikate tamaa. Hata wengine pia walikutana na changamoto wakati wanaomba. Siku zote amini kuwa, aliyewawezesha wengine kupata ndiye atakayekuwezesha wewe kupata.
7. Jihadhari na **utapeli**, kwenye uombaji wa ufadhili kuna utapeli pia hivyo hakikisha unahakiki ufadhili/chuo husika ili kuepuka kutapeliwa. Kumbuka kuwa si kila tangazo la ufadhili/udahili ni la kweli.
8. Epuka kunakili taarifa za mitandaoni na badala yake andika maandiko yako au ikibidi kuchukua taarifa za mtandaoni basi mtaje na muandishi ili kuepuka kosa la kunakili (plagiarism). Kuwa mkweli katika maelezo yako wakati unaandaa Wasifu binafsi (CV) au mpango wa masomo (Study plan) au barua ya motisha (motivational letter) au insha (essays). Mara nyingi uitwapo katika usaili, baadhi ya maswali huulizwa kulingana na taarifa ulizojaza katika nyaraka nilizotaja hapo awali, sasa kama umedanganya itakuwa vigumu kwako kujitetea.
9. Unashauriwa kuomba fadhili nyingi kadiri uwezavyo kulingana na vigezo unavyokidhi. Hata hivyo, ushauri wangu ni kuchagua fadhili zisizopungua 3 na zisizozidi 10 na kuhakikisha unazifatilia kwa umakini mkubwa sana. Kumbuka kuwa, kuomba fadhili nyingi bila kufata maelekezo husika au kukidhi vigezo husika hakukuongezei nafasi ya kupata badala yake nafasi ya kupata inaongezeka iwapo utafata maelekezo/vigezo husika hata kama utaomba ufadhili mmoja tu. (Hoja sio wingi wa kuomba fadhili nyingi, bali kinachosisitizwa ni kufata maelekezo husika kisha kuomba fadhili husika)
10. Tafadhali tambua kuwa uombaji wa fadhili au vyuo unahitaji umakini wako. Usiharakishe kutuma maombi kabla hujasoma maelekezo husika. Mfano, kuna baadhi yetu walifika mpaka chuo husika walichoomba wakidhani kuwa fadhili waliyopata ni ya kulipiwa kila kitu (fully funded) hali yakuwa ni ya kulipiwa baadhi (partially funded) na hivyo kupelekea kusoma kwa shida, kupata msongo wa mawazo na athari nyengine. Yasingewapata haya laiti wangelisoma maelekezo husika ya fadhili/chuo kabla ya kuomba.
11. Nafahamu UGUMU unaopatikana wakati wa kufatilia fadhili mbalimbali lakini JITAHIIDI ufanye maombi wewe mwenyewe na sio kufanyiwa na mtu au wakala. Hii itakurahisishia wakati wa usaili (interview) kwa kuwa utakuwa unajuwa ulichokiandika wakati unafanya maombi.

**INDHARI:** Lengo la muongozo huu ni kukupa mwanga wa namna ya kuomba ufadhili au chuo husika. Mwandishi hatoi huduma ya kufanyia watu maombi ya ufadhili wa aina yeyote ile, lakini yupo tayari kukusaidia pale utakapokwama kwa fadhili ambazo ana uzowefu nazo. Aidha maoni yaliyoandikwa humu hayatokani na taasisi au bodi ya ufadhili husika bali yanatokana na uzoefu wa mwandishi katika ufadhili husika.

WananchiForum

## MAELEZO JUU YA UFADHILI WA COMMONWEALTH MASTER'S SCHOLARSHIPS.

### UTANGULIZI.

Commonwealth scholarships ni scholarships ambazo hutolewa na Kamisheni ya Ufadhili ya Commonwealth (Commonwealth Scholarship Commission-CSC) iliyopo nchini Uingereza kupitia ofisi ya Maendeleo, Mambo ya nje na Jumuiya ya Madola (UK Foreign, Commonwealth and Development Office-FCDO). Ufadhili huu ulianza rasmi mwaka 1960 na mpaka sasa wanufaika Zaidi ya 31,000 kutoka nchi mbalimbali wamenufaika na ufadhili huu. Lengo kuu la fadhili hizi ni kuwasaidia raia hodari kutoka nchi za Jumuiya ya Madola kuweza kusoma katika vyuo vya Uingereza na kuweza kuleta mabadiliko na athari za maeneleo endelevu hasa katika nchi zao.

Kwa sasa scholarship hizi zipo za aina 7 ambazo ni:

1. [Commonwealth Master's Scholarships](#)
2. [Commonwealth Shared Master's Scholarships](#)
3. [Commonwealth Distance Learning Master's Scholarships](#)
4. [Commonwealth Split-site PhD Scholarships](#)
5. [Commonwealth PhD scholarships](#)
6. [Commonwealth Professional Fellowships](#)
7. [High-income PhD Scholarships](#)

Kati ya hizo 7, Watanzania wana kidhi vigezo vya kuomba (Tanzania is an eligible country) 6 kati yake (namba 1-6). Tafadhali bonyeza aina husika ya scholarship ili kujua zaidi. Pia kuna scholarship nyengine ijulikanayo kama [Queen Elizabeth Commonwealth Scholarship](#) ambayo watanzania pia wanakidhi kuomba ingawa ina jina la Commonwealth lakini haipo chini ya Kamisheni ya Commonwealth (CSC) badala yake ipo chini ya Jumuiya ya Vyuo vilivyo chini ya Jumuiya ya Madola (Association of Commonwealth Universities). SUZA na UDSM na vyuo vyengine ni miongoni mwa vyuo vilivyomo katika Jumuiya hii.

Katika muongozo huu tutazungumzia aina ya kwanza ya scholarship kati ya saba zilizo chini ya CSC.

### UTANGULIZI JUU YA COMMONWEALTH MASTER'S SCHOLARSHIP.

Huu ni ufadhili unaolipia kila kitu (fully funded scholarship) unaotolewa na CSC kupitia ofisi yake ya Mambo ya nje, Jumuiya ya madola na maendeleo kwa kushirikiana na vyuo vikuu vya Uingereza vilivyoingia makubaliano na CSC.

Ufadhili huu ni miongoni mwa fadhili zenye ushindani mkubwa zaidi duniani. Mchakato wa ufadhili huu hutumia wastani wa miezi nane takriban, kuanzia siku ambayo dirisha la maombi linafungwa mpaka wanufaika wanawasili nchini Uingereza kwa ajili ya kuanza masomo. Kwa kawaida dirisha la maombi hufunguliwa mwezi wa Septemba na kufungwa Octoba kila mwaka.

Tambua kuwa dirisha la maombi likifunguliwa, maombi ambayo hupokelewa na kuchakatwa ni kwa ajili ya mwaka wa masomo unaoanza mwaka unaofata. Mfano, kwa mwaka huu 2024, dirisha limeshafunguliwa tangu tarehe 10 Septemba hivyo iwapo utafanikiwa kupata ufadhili huu masomo yanatarajiwa kuanza Septemba/Oktoba 2025. (yaani ukiomba mwaka huu maana yake unaomba kwa mwaka wa masomo 2025/2026 na sio 2024/2025)

Ufadhili huu unahusisha kwenda kusoma masomo ya shahada ya uzamili (Master's degree) nchini Uingereza kwa muda wa mwaka mmoja.

**Baadhi ya faida za ufadhili huu ni pamoja na:**

- + Kusoma shahada ya uzamili ndani ya mwaka mmoja katika chuo kikuu cha Uingereza
- + Kulipiwa ada ya masomo
- + Kulipiwa pesa za utafiti
- + Kulipiwa pesa za nguo za joto (Warm clothes allowance)
- + Kurejeshewa pesa ulizotumia wakati unafanya TB test
- + Kulipiwa Tiketi za ndege kwenda na kurudi nchini Uingereza.
- + Kulipiwa gharama za Visa na bima ya afya
- + Kulipiwa posho la kujikimu la kila mwezi uwapo Uingereza
- + Kushiriki matukio mbalimbali yatakayosimamiwa na Commonwealth
- + Kuungana na wanufaika wengine wa Commonwealth zaidi ya 31,000
- + Kujifunza tamaduni mpya ya watu wa Uingereza au watu wengine wanufaika wa Commonwealth

**Mchakato wa ufadhili huu ni kama ifuatavyo:**

Uombaji wa ufadhili huu wa Commonwealth Master's hufanywa kwa kupitia Uteuzi (Nomination) unaofanywa na wateuzi mbalimbali (Nominating agencies) walioingia makubaliano na CSC. Baada ya maombi ya ufadhili huu kuteuliwa na wateuzi ndipo yatapelekwa katika Kamisheni ya CSC ambayo ndio itakayoamua kukupa ufadhili huu iwapo umefaulu vizuri. Jedwali lifuatalo kwa ufafanuzi zaidi:

Kufunguliwa kwa dirisha la maombi na kuanza kupokelewa kwa maombi ya ufadhili	Tarehe Septemba 10, 2024
Kufungwa kwa dirisha la maombi na mwisho wa kupokelewa kwa maombi ya ufadhili.	Tarehe 15 Oktoba 2024
Maombi huchakatwa na wateuzi (Nominating agencies) na wapendekezwa (nominees) huwasilishwa kwa CSC,	Kuanzia Oktoba 16 mpaka Disemba 2024
Maombi huchakatwa na CSC	Kuanzia Januari mpaka Mei 2025
Majibu kutoka CSC	Katikati au mwishoni mwa Mei 2025
Wachaguliwa hupewa mda wa kukamilisha vitu ambavyo havikutimia kama vile Barua ya	Katikati au mwishoni mwa Mei 2025 mpaka Septemba.



udahili (Unconditional offer) kutoka chuo cha Uingereza.	
Masomo huanza	Septemba/Octoba 2025

Kama mchakato unavoonesha hapo juu, maombi ya ufadhili huu huwa wazi kwa muda mfupi wa takriban siku 35 tu na majibu hutolewa baada ya miezi kadhaa kupita mpaka Mei 2025. Utafurahia kutokufanya interview (si kwa nominating agent wala kwa CSC labda chuo utakachoomba na si vyote vitakavyokufanyia interview) Nchi nyengine kama Nigeria, Nominating agency wao hufanya interview. Lakini usisahau kuwa utalazimika kuandika insha 11 zenye ukomo wa maneno baina ya 100 mpaka 500 zenye maelekezo maalum ya kuyazingatia ili uweze kutuma maombi yako. Baada ya dirisha la maombi kufungwa Octoba 15 basi jivinjari na usubiri majibu Kuanzia Mei 2025.

### **WATEUZI (NOMINATING AGENCIES)**

Kwa Tanzania, wateuzi walioingia makubaliano na CSC wanapatikana kupitia kiunganishi hiki <https://cscuk.fcdo.gov.uk/national-nominating-agencies/> Pia kuna baadhi ya Mashirika yasiyo ya Kiserekali (NGO's) ambayo pia yanaweza kufanya uteuzi. Tafadhali tembelea hapa <https://cscuk.fcdo.gov.uk/ngos/> ili kujua zaidi kuhusu NGO hizi.

Kwa upande wangu, nilitumia Nominating agency wetu ambaye ni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya Tanzania. Mawasiliano yao yapo katika kiunganishi cha Nominating agency hapo juu au unaweza ukatumia haya:

Officer, Department of Higher Education

PO Box 10

Dodoma

Tanzania

Tel: +255 754 206 860

Email: [clement.sanga@moe.go.tz](mailto:clement.sanga@moe.go.tz)

Website: [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)

Kwa upande huu wa wizara, wakati unafanya maombi ya scholarship (tutaona huko mbeleni) utachagua Wizara ya Elimu kama ndio Nominating agency wako. Huhitaji kutuma/kufanya maombi mengine kwenda wizarani kwa kuwa wao Wizarani watayaona na kuyapokea maombi yako kupitia application portal ya CSC. Wakati nafanya maombi Sep 2023, nilipiga namba hiyo hapo juu na nilimuuliza Mhusika kuhusu namna ya kufanya maombi ya ufadhili huu kwa nominating agency kama ilivosisitizwa katika tovuti ya CSC ("As well as applying to the CSC, applicants must apply to a **nominator**") na alinambia sihitajiki kutuma maombi wizarani na sikutuma wizarani na waliweza kuiteua. Hata hivyo, iwapo utapenda unaweza ukatuma Pdf moja uliyounganisha ile completed application form ya CSC pamoja na viambatanisho vyengine kwenda katika email tajwa hapo juu.

Ni muhimu kufahamu kuwa ufadhili huu ni miongoni mwa fadhili zenye ushindani zaidi duniani, hivyo kuongeza nafasi zaidi ya kupata ninakushauri uombe na scholarship



nyengine kama Chevening, Commonwealth shared, Distance learning, Queen Elizabeth, Erasmus mundus, Chinese Government (MOE, MOFCOM, na hata za nyuo) na scholarship nyengine pindi madirisha yao ya maombi yakifunguliwa.

Pia tunashauriwa kutumia NGO's kama [Commonwealth Disabled People's Forum \(CDPF\)](#), [The Commonwealth Equality Network \(TCEN\)](#) and [Forum for African Women Educationalists \(FAWE\)](#) ili kuongeza nafasi zaidi za kupata ufadhili huu. Tafadhali tembelea NGO's husika ili kujua mahitajio na vigezo vyao (requirement and eligibility) ili waweze kukuteua.

**Jambo la kuzingatia: Unaweza ukateuliwa na Nominating agency lakini ukafeli CSC** au unaweza ukashindwa kuteuliwa na Nominating agency na hivyo maombi yako yasifike CSC. Hakikisha unatuma maombi yaliyo na ubora ili kujihakikishia nafasi zaidi. Kumbuka pia kila Nominating agent ana kiwango maalum cha nominees anaotakiwa awateue (kama inavyoelekezwa katika tovuti ya CSC "Participating nominators put forward an ***agreed number of candidates*** to the CSC for consideration.") Hivyo basi inawezekana ukakidhi vigezo vyote lakini idadi maalum ya nominees ikawa imeshafikiwa na hivyo kupelekea kutoteuliwa-Usivunjike moyo na hili, omba mara nyengine tena au omba fadhili nyengine.

Pia kuteuliwa na Nominating agency sio kigezo cha kupata scholarship, CSC nao wana vipimo vyao (Evaluation criteria) ambavyo tutaviona huko mbeleni. "Selections are made from the pool of nominations. Candidates are asked to note that **a nomination is no guarantee of selection.**"

**Ushauri kutoka kwa Wahusika Wizarani:** Baada ya kufanikiwa kupata ufadhili huu, niliwasiliana na email ya wizara iliyopo hapo juu ili kutoa shukran zangu kwao kwa kuniteua na hatimae CSC kunipa ufadhili wao. Wahusika kwa pamoja waliniusia kuwashajihisha watanzania wenye sifa waombe wengi zaidi na kwa kuzingatia mahitajio ya ufadhili huu kama kuhakikisha unakamilisha maombi ndani ya muda, kupandisha (upload) nyaraka zoote zinazotakiwa katika portal ya maombi na kujibu vizuri insha 11 zilizopo katika portal. Hivyo, kupitia Muongozo huu salamu hizi nimezifikisha kutoka kwa Nominating agent wetu.

**TANBIHI:** Maombi ya ufadhili huu ni lazima yapitie kwa wateuzi ndipo yawasilishwe CSC. CSC haipokei maombi ya muombaji moja kwa moja.

## VICEZO STAHIKI VYA UFADHILI HUU (ELIGIBILITY CRITERIA)

- ✚ Kuwa raia au mkimbizi katika nchi zinazotambuliwa kama nchi wanachama wa Jumuiya ya madola (Commonwealth countries), **Tanzania ni mojawapo.**
- ✚ Kujikubalisha kurudi nchini mwako baada ya kumaliza masomo ya shahada ya uzamili nchini Uingereza.
- ✚ Kuwa tayari kuanza masomo ya Shahada ya Pili mwezi Sept 2025.
- ✚ Kuwa na Shahada ya kwanza kwa ufaulu wa angalau Upper second class (GPA >3.4) au ***iwapo utakuwa na ufaulu chini ya Upper second class*** basi uwe na shahada ya pili katika fani husika. Kwa waombaji wenye ulemavu (wa aina yoyote) wao wanaweza kuomba hata kama ufaulu wao ni chini ya Upper second Class na hata kama hawana shahada ya pili. Waombaji hawa (wenye Ulemavu) wanashauriwa kutumia NGO ya [Commonwealth Disabled People's Forum \(CDPF\)](#) kupitishia maombi yao ili kuongeza nafasi Zaidi.
- ✚ Kutokuwa na uwezo wa kusoma shahada ya uzamili katika vyuo vya Uingereza.
- ✚ Kutuma nyaraka zote hitajika katika muundo uliopendekezwa.

## NYARAKA ZINAZOHITAJIKA.

- ✚ Nyaraka za kitaaluma (Academic certificates and transcripts)
- ✚ Wadhamini wawili wa kitaaluma (Two academic referees)
- ✚ Hati/pasi ya kusafiria au Kitambulisho cha NIDA (iwapo utakuwa huna pasi ya kusafiria, lakini anza kufatilia uwe nayo)
- ✚ Barua ya udahili kutoka chuo cha Uingereza-hii kwa tarehe za mbeleni baada ya kuchaguliwa na CSC.

## UCHAGUZI VIGEZO VYA UCHAGUZI (CSC SELECTION PROCESS AND CRITERIA)

Tafadhali zingatia mchakato huu kwa kuwa ndio utakaokusaidia kufanikiwa kupata ufadhili huu. Uchaguzi wa waombaji wa ufadhili huu unafanywa na CSC baada ya waombaji kuteuliwa na Nominating agencies. Maombi ya waombaji hupewa alama (score graded) kulingana na vitu vifuatavyo:

- ✚ Uhodari wa kitaaluma (Academic merit)
- ✚ Ubora wa mpango wa masomo (Quality of study plan)
- ✚ Uwezo wa kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika nchi yako (Potential impact on the development of the candidate's home country)

Jumla ya alama (overall grade score) inayotakana na vitu hivyo vitatu ndio itakayokufanya upate scholarship au ukose. Kulingana na ugawanyaji wa alama hizi, inamaanisha kuwa unaweza ukapata alama nyingi kwenye upande wa Academic merit mfano GPA kubwa, lakini ukapata alama ndogo katika Study plan na development impact (hizi utapimwa wakati unajibu zile insha 11) na hivyo kupelekea kupata alama ya jumla iliyo ndogo na hivyo kushindwa kupata ufadhili huu. Vilevile unaweza ukapata alama ndogo kwenye upande wa Academic merit mfano GPA ndogo (lakini ni kubwa kuliko 3.4), lakini ukapata alama kubwa katika Study plan na development impact (hizi utapimwa wakati unajibu zile insha 11) na hivyo kupelekea kupata alama ya jumla iliyo kubwa na hivyo kufanikiwa kupata ufadhili huu.

Jedwali hili hapa chini limeelezea Zaidi namna ya ugawanyaji wa alama kwa Nyanja 3 kama nilivoinisha hapo juu. Zingatia kuwa Primary indicators zina kipaumbele zaidi ya secondary indicators.

## Grading system for assessment of applications

### for FCDO-funded commonwealth scholarships tenable in the United Kingdom

Grade	Academic merit	Quality of Research proposal (doctoral)	Quality of Study plans (Masters)	Development impact
Grading criteria	<p><b>Primary Indicators</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Examination results</li> <li>• Academic transcripts</li> <li>• Tutors' and referees' reports</li> </ul> <p><b>Secondary Indicators</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Academic prizes or awards</li> <li>• Other relevant academic achievements</li> <li>• Publications, where appropriate</li> </ul>	<p><b>Primary Indicators</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Clear abstract of what the candidate wants to research</li> <li>• Extent to which the work programme has been well researched (including references to key literature); and the extent of engagement with the host supervisor</li> <li>• Quality of the research proposal, including innovation and relevance to current research in the chosen field and to development policy</li> </ul> <p><b>Secondary Indicators</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Clarity of expression.</li> <li>• Feasibility of proposed research</li> <li>• Likelihood of completion within three years</li> </ul> <p><b>For Split-Site Awards:</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Relevance of work in UK to PhD</li> <li>• Evidence of strong research link with UK institution</li> </ul>	<p><b>Primary Indicators</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Statement of what the candidate wants to learn and how it relates to their objectives</li> <li>• Extent to which the proposed course and institution of study have been well researched (including specific options and dissertation topics, where appropriate) and presented</li> </ul> <p><b>Secondary Indicators</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Existing offer of admission to the course</li> <li>• Clarity of presentation</li> </ul>	<p><b>Primary Indicators</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Extent of the need: how the plan of study/research relates to development in the sector and country</li> <li>• Expected outcomes, the projected timeframe to achieve them and potential beneficiaries</li> <li>• The way and extent to which the candidate proposes to apply new skills and qualifications; how does this relate to development</li> </ul> <p><b>Secondary Indicators</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Reference to a national development priority or capacity shortage</li> <li>• Reference to the selected CSC theme</li> <li>• Extent of the benefit: how the impact of the work might be measured</li> <li>• Past demonstrable commitment to 'development' agendas through voluntary work.</li> <li>• Leading or participating in relevant projects or programmes</li> </ul>

## HATUA ZA KUFANYA ILI KUOMBA UFADHILI HUU.

Awali kabla ya yote tembelea kiunganishi hiki ili kusoma Ushauri kwa waombaji kutoka kwa Kamati ya chaguzi ya CSC <https://cscuk.fcdo.gov.uk/advice-for-applicants/>

Pia tembelea ukurasa wa majibu ya maswali yaulizwayo mara kwa mara (FAQs) ili ujifunze zaidi <https://cscuk.fcdo.gov.uk/commonwealth-scholarships-frequently-asked-questions/>

Huhitaji kuwa na uzoefu wa kazi ili kuomba ufadhili huu. Pia kwa ngazi ya Masters hata kama huna machapisho (publications) unaweza ukaomba, kumbuka kuweka tuzo (awards) kama unazo. Mfano kama Best student award, leadership award, membership award nk.

Ufadhili huu hautoi ufadhili kwa shahada za Usimamizi wa biashara (Master of Business Administration programs), hivyo chagua kada mbadala zisizokuwa MBAs ili uweze kuomba ufadhili huu.

Ufadhili huu hutolewa kwa kuzingatia maudhui 6 (6 CSC Development themes) ambapo itakupasa uandishi wako wa insha uzingatie moja ya maudhui haya. Pia itakupasa kuchagua Sustainable Development Goals SDGs 3 kati ya zile 17, zinazoendana na kada uliyochagua na malengo yako (career plans). Kupitia link hii unaweza ukasoma zaidi kuhusu maudhui haya <https://cscuk.fcdo.gov.uk/csc-development-themes/> Ni lazima insha zako uziunganishe kwa namna gani zinaendana na mojawapo ya maudhui haya. Maudhui haya ni kama ifuatavyo (boneza kila maudhui ili kupata maelezo yake):

- ✚ [Science and technology for development](#)
- ✚ [Strengthening health systems and capacity](#)
- ✚ [Promoting innovation and entrepreneurship](#)
- ✚ [Strengthening global peace, security and governance](#)
- ✚ [Strengthening resilience and response to crises](#)
- ✚ [Access, inclusion and opportunity](#)

Fuata hatua hizi ili kuweza kuomba ufadhili huu:

- ✚ Hatua ya kwanza: Chagua kada 3 za shahada ya uzamili katika vyuo vya Uingereza. Tembelea vionganishi vifuatavyo (chagua kimojawapo)
  - [Study UK](#) – British Council website, with guidance for international students and a course and institution search
  - [Steps to Postgraduate Study](#) – a guide to asking the right questions about taught postgraduate study in the UK
  - [Postgrad.com](#) – information for postgraduate students, with a course search
  - [Prospects](#) – information on postgraduate study in the UK
  - [Research Excellent Framework 2021 results](#) – results of a system for assessing the quality of research in UK higher education institutions

- [UCAS Postgraduate](#) – guidance on how to find and apply for a postgraduate course
- [Discover Uni](#)– the official website for comparing UK higher education course data
- [UKCISA](#) (UK Council for International Student Affairs) – advice for international students on choosing a course of study

✚ Hatua ya pili: Hakikisha vyuo vyote 3 ulivyochagua kada zako vipo katika list ya vyuo vilivyoingia makubaliano na CSC. Ili kujua hilo tafadhali tembelea kiunganishi kifuatacho <https://cscuk.fcdo.gov.uk/uk-universities/> Kumbuka kuanza kufanya maombi katika kada na nyuo ulivyoainisha mara tu baada ya kumaliza maombi ya Commonwealth.

✚ Hatua ya tatu: Andaa nyaraka zako za kitaaluma na taarifa zako za wadhamini. (tafadhali tembelea kiunganishi hiki <https://www.chevening.org/resource-hub/guidance/references/>) kumbuka kuwa nyaraka laini ya vyeti vyako halisi sio nakala ndio vinavyohitajika hapa (yaani scan vyeti na transcript halisi na sio nakala pia huhitaji kuvipiga muhuri wa mwanasheria kwa kuwa umescan nyeti halisi na sio nakala).

✚ Hatua ya nne: Kamilisha maombi yako na utume kupitia kiunganishi <https://fs29.formsite.com/m3nCYq/mdvukkr8dy/index> Hapa utapaswa kujibu insha 11 (essays) kwa ukomo wa maneno kati ya 100 hadi 500 kwa kila moja ambazo ni:

Commonwealth Scholarships in the UK are funded by the UK Foreign, Commonwealth & Development Office (FCDO). An important selection criterion is the potential contribution that you will make to international development if you are awarded a scholarship. Provide a Development Impact statement in 4 parts explaining:

1. How your proposed study relates to: (max 200 words)
  - a) development issues at the global, national and local level?
  - b) development issues connected to your chosen CSC development theme and the wider sector?
2. How you intend to apply your new skills and qualification when you return home? You may wish to reference innovation and application of knowledge at a global, national or local level, and to include intended methodologies and implementation strategies. (max 100 words)
3. What you expect will change in development terms following your studies, including: (max 250 words)
  - a) the outcomes that you aim to achieve?
  - b) the timeframe for their implementation?
  - c) who the beneficiaries will be?



4. How will the impact of your work be best measured and evidenced? Please include details of what indicators are used to measure this impact. You may wish to detail small and incremental changes as well as more significant goals. (max 100 words)

The selection panel will want to understand how your proposed study will assist you in your career.

Describe the skills that you expect to gain from this scholarship, and your career plans once you return home afterwards.

5. Objectives during the award. (max 250 words)

6. Career plans in the 5 years following the award. (max 250 words)

7. Longterm career plans. (max 250 words)

8. Provide a short outline of your proposed study/research. This should be written for an audience that does not have any prior knowledge of the subject, and must not be overly technical. Any abbreviations or specialist terms must be explained. Study outline (max 125 words)

9. Provide a detailed plan of your proposed study. The selection panel will want to understand why you have selected your proposed courses and universities. You should remember that, although the selection panel will be well informed, they are not likely to be specialists in your subject. (max 300 words)

Describe clearly:

- why you have chosen your proposed courses and universities and why you want to undertake this study in the UK
- what it is that you are looking for in a course and how your chosen courses relate to your objectives
- any dissertation topic you have in mind

10. The CSC encourages applications from candidates who have faced significant disadvantage or personal barriers to higher education or are under-represented in their field of study/workplace.

Please summarise the ways in which your personal background has encouraged you to want to make an impact in your home country.

You may wish to highlight any areas where you have already made significant contributions, including overcoming personal or community barriers in accessing higher education or within your field.

Personal statement (max 500 words)



11. Summarise the ways in which you have engaged in voluntary activities and the opportunities you have had to demonstrate leadership  
Voluntary and leadership experience (max 500 words)

Insha hizi ndio moyo wa maombi yako, hivyo jitahidi kufanya vizuri wakati unajibu insha hizi. Nitaelezea namna ya ujibuji wake huko mbeleni.

- ✚ Hatua ya tano: Baada ya kutuma maombi yako, subiri majibu. Iwapo utafanikiwa utapokea email kutoka CSC Mei 2025.
- ✚ Hatua ya sita: Fanya maombi katika zile kada 3 ulizochagua katika vyuo vya Uingereza na hakikisha unapata barua ya udahili isiyo na masharti (unconditional offer) kabla ya Septemba 2025. Nitaelezea namna ya kufanya maombi katika vyuo vya Uingereza huko mbeleni.
- ✚ Hatua ya saba: Iwapo utafanikiwa katika hatua tano na ya sita, hongera juu yako. Usisahau kuwasaidia wataanzania wengine na wao waweze kufanikiwa kama ulivyofanikiwa wewe.

## JE NI LAZIMA UWE NA CHETI AU UFANYE MTIHANI WA KIMATAIFA WA KIINGEREZA (IELTS AU TOEFL)?

Jambo jema ni kuwa Ufadhili huu wa Commonwealth hauna kigezo cha ulazima wa kuwa na cheti cha kuthibitisha ufasaha wa lugha ya kiingereza. Hata hivyo, uandishi wako wa insha utatumika kukupima uwezo wako katika kuandika na kufikisha ujumbe kwa kiingereza.

Aidha vyuo vingi vya Uingereza vinahitaji vyeti hivi vya ufasaha hasa IELTS. Nikutoe wasiwasi kuwa unaweza kupata udahili kutoka katika vyuo vya Uingereza bila ya kuwa na vyeti hivi hata kama chuo husika kimeweka hitajio la cheti cha Kiingereza cha IELTS au TOEFL (Nitaelezea huko mbeleni).

Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kuwa iwapo utafanikiwa kupata ufadhili huu, masomo pamoja na mazingira yako yatakuwa ni kwa lugha ya kiingereza kwa asilimia 100. Ni juu yako kuhakikisha unajua lugha hii kwa ufasaha ili kuepuka madhara yasiyo ya lazima kama vile kufeli na msongo wa mawazo.

## NAMNA YA KUJIBU INSHA 4 ZA CHEVENING NA MIFANO

Kama nilivyotangulia kusema hapo awali kuwa insha hizi ndio moyo wa maombi yako katika ufadhili huu. Ukiharibu katika insha ndio umeshaharibu maombi yako. Tafadhali tumia muda mwingi kuandaa insha hizi. Una takriban siku 30 za kuandaa insha hizi kabla ya kufungwa kwa dirisha la maombi ya ufadhili huu. Tafadhali tembelea kiunganishi hiki [https://youtube.com/playlist?list=PLHZYXfQI6b\\_7\\_QxLRjpVTV6phytPIuGo&feature=shared](https://youtube.com/playlist?list=PLHZYXfQI6b_7_QxLRjpVTV6phytPIuGo&feature=shared) ili uweze kujifunza vizuri namna bora ya kujibu insha hizi. Tafadhali chukua kalamu na daftari uwe unaandika vitu muhimu wakati unapitia kiunganishi hiki. Ni matumaini yangu kuwa iwapo utapitia kiunganishi hivi, utafanikiwa kupata ufadhili huu (Usisahau kutumia mitandao kama Grammarly ili kurekebisha makosa ya kiuandishi wakati unaandika insha zako).


Nilipoandaa Muongozo wa Chevening, baadhi ya waombaji walihitaji niwape insha za waliofanikiwa kupata ufadhili wa Chevening ili waone kile walichokiita "sample" Kwa bahati mbaya sikuwapa na sitoweza kuwapa insha za waliofanikiwa kupata Ufadhili huu ikiwemo insha zangu. Sababu kuu ni kukujenga zaidi kwa sababu nimeshakupa kiunganishi hapo ambacho utajifunza namna ya kuziandaa insha zako. Pia unaweza ukafatilia tutorial nyengine za youtube zinazozungumzia ufadhili huu ili kukujenga zaidi. Iwapo nitaziweka wazi insha za waombaji waliofanikiwa ikiwemo zangu, kuna hatari kubwa nikaharibu badala ya kusaidia kwa kuwa wengi wetu aidha tutanakili baadhi ya insha hizi au tutaegemea katika muundo/mawanda ya muombaji aliyefanikiwa na hivyo kuingia katika kosa la plagiarism au same structure essay format ijapokuwa content ni tofauti. Hivyo kuepuka hilo, ni bora kufundishwa mbinu za kuvua kuliko kupewa samaki.

Ushauri wangu kuhusu insha hizi ni:

- ✚ Kufanya utafiti wa kina kuhusu kada unazotaka kuomba, na wakati unaandaa study plan hakikisha unahusisha some key modules na Tutors wake.
- ✚ Husisha takwimu halisia katika insha zako
- ✚ Egemeza malengo yako (career plans) na Sustainable Development Goals
- ✚ Fuatilia kuhusu development projects zinazofanyika na zinazotarajiwa kufanyika na uhusishe vipi masomo yako ya shahada ya Uzamili nchini Uingereza yatakupelekea kusaidia au kushiriki katika kufanikisha maendeleo katika jamii.
- ✚ Pembua changamoto zilizopo katika jamii yetu kisha ihusishe na elimu yako na uwezo wako wa sasa kisha elezea kwa namna gani baada ya kupata elimu ya juu ya Uzamili kutoka Uingereza itakuwezesha kutatua changamoto hizo.
- ✚ Mara zote husisha masuala ya jinsia (gender inclusion) katika malengo yakon na onesha kuwa unashajihisha usawa wa kijinsia.
- ✚ Kwa bahati mbaya (samahani sana kwa hili), iwapo ni mvivu katika kusoma na kufatilia mambo/maelekezo basi ufadhili huu unaweza usikufae. Muundo wa ufadhili huu unakujenga uweze kujitegemea (self independent) hivyo kuna mambo

hayatokuwa wazi sana kama tulivozoea, na itakupasa ujitume zaidi ili uweze kuyang'amua hasa kabla ya kupata ufadhili huu.

Jipinde sasa ili ujihakikishie kupokea email hii, ifikapo Mei mwakani!




## NAMNA YA UOMBAJI HATUA KWA HATUA

Fungua kiunganishi hiki ili kuanza maombi ya ufadhili huu

<https://fs29.formsite.com/m3nCYq/mdvukkr8dy/index>

Chagua nchi (Tanzania), kisha chagua Next



COMMONWEALTH SCHOLARSHIPS


COMMONWEALTH SCHOLARSHIP  
MASTERS APPLICATION 2025

What is your Nationality or Residency? \*

Tanzania

Save Progress Next >>

Utafunguka ukurasa wa kujisajili, chagua New User kisha jaza email na password, kisha Next. Utafunguka ukurasa wa Eligibility and Due Diligence chagua Yes.



4% Complete

**Eligibility and due diligence**

By September 2025, you must hold either a first university degree of at least upper second class (2:1) honours standard or a second class (2:2) university degree and a relevant postgraduate qualification (usually a Master's degree) to meet the academic eligibility criteria for this scholarship.

Your personal information will be used to conduct necessary due diligence checks to the CSC's satisfaction, before the CSC proceeds with any type of formal agreement or contractual relationship. In most cases, the due diligence checks will be straightforward, however further information may be requested, so we ask for your full co-operation to speed up the process.

If you do not agree to your personal data being used for the purpose of conducting due diligence, unfortunately you will not be able to proceed further with the application process.

Do you meet the academic eligibility criteria and agree to the due diligence checks? \*

☒ no ☐ yes

<< PREVIOUS SAVE PROGRESS NEXT >>

Katika Nomination chagua Nominator wako

13% Complete

**Nominator**

PLEASE NOTE that it is your responsibility to research your eligibility to apply via this nominator. Check the [CSC website](#) for details of all nominators and contact the individual nominator for their specific eligibility criteria. If you do not choose the correct nominator neither the nominator nor the CSC is under any obligation to consider your application.

**Nominating Agency in Tanzania \***

Tanzania : Ministry of Education, Science and Technology

<< PREVIOUS    SAVE PROGRESS    NEXT >>

Applications with references must be submitted by 16:00 (GMT) on 15 October 2024

Baada yah apo jaza form kadiri inavyoelekeza. Iwapo utahitaji kuendelea baadae bonyeza Save progress kisha log out kwa kufunga browser tab. Utatumia email/username yako na password kurudi tena iwapo utataka kuendelea. Waakati unajaza taarifa za chuo Kumbuka kuwa I ni sawa na 1<sup>st</sup> class, Iii ni sawa na Upper Second class, Iiii ni sawa na Lower second class na Pass ni sawa na Pass vile vile.

Katika ukurasa wa Development impact, chagua maudhui moja kati ya 6 (one out of 6 CSC development's themes) kisha chagua SDG 3 zenye kuendana na kada yako na malengo yako. Kisha utanza kujibu insha zako. Tafadhali rejea katika Hatua za kufanya ili kuomba ufadhili huu ili kuyaona maswali ya insha.

Katika ukurasa wa Proposed study in the UK, jaza kada 3 na vyuo 3 ulivyochagua kama nilivoelekeza katika Hatua za kufanya ili kuomba ufadhili huu. Kisha utajaza mawasiliano (contact details) ya kila chuo katika sehemu iliyowekewa ukomo wa maneno 100.

Endelea na portal mpaka katika ukurasa wa kupakia (upload). Pakia nyaraka zinazohitajika kisha tuma maombi yako. Kila la kheri!

## KUHUSU REFEREES.

Tafadhali ongea na uwaombe referees wako mapema na wajulishe kuwa unatarajia kuomba Ufadhili huu na vyuo vya Uingereza. Pia wajulishe kuwa kuna muongozo juu ya uandishi wa reference/recommendation letter za Commonwealth katika kiunganishi hiki <https://cscuk.fcdo.gov.uk/scholarships/commonwealth-masters-scholarships/> au kwa ufupi mwambie afate maelekezo haya:

When completing the references, referees should be asked to comment as fully as possible on the applicant, keeping in mind the following points for inclusion, as appropriate:

- ✚ How long, and in what capacity, the referee has known the applicant.
- ✚ The referee's views on the applicant's suitability for the proposed Scholarship and the need for the particular subject of study in the UK.
- ✚ Information on how, and to what extent, the applicant has shown ability in terms of:
  - capability to grasp concepts and reason analytically;
  - capacity for original thought;
  - and motivation and perseverance in achieving objectives.
- ✚ Assessment of the applicant's particular strengths and weaknesses.
- ✚ The applicant's potential to impact development in their home country.
- ✚ Any other general qualities which the referee considers would make the applicant a good recipient of a Scholarship.

Kumbuka kuwa referee wako anatakiwa akuandikie recommendation letter iliyozingatia maelekezo yah apo juu kisha akupe, wewe ndio utaipandisha (upload) katika portal ya CSC wakati unaomba.


**Tunawashukuru referees wote ambao wamekuwa nasi bega kwa bega kutusaidia katika maombi ya fadhili na vyuo mbalimbali. Kwa heshima kabisa nimshukuru Dr Robert Katikiro, Dr Maliwaza Mbwana na Dr Pazi Semili kwa msaada wao mpaka nimefanikiwa kupata ufadhili huu. MwenyeziMungu awabariki nyinyi na familia zenu.**




## NAMNA YA KUOMBA VYUO VYA UINGEREZA.

Kuchagua kada bonyeza kiunganishi hiki [Study UK](#) au kiunganishi chengine kama nilivoainisha huko juu katika mwongozo huu.

Andika jina la kada unayotaka kuomba na level ya elimu kisha tafuta (search).



Mimi nimetafuta kwa kuandika "Agricultural economics" na level ya elimu nimeweka Master's na matokeo yakaja hivi:



Nimehakiki katika vile vyuo vilivyoingia makubaliano na CSC na nimegundua kuwa University of Reading kipo hivyo naendelea na hatua ya mbele. Bonyeza kada husika au 'read more' ili upate maelezo na mahitaji ya kada na mengineyo, mfano kama hivi:

search-study-uk.britishcouncil.org/course/details.html?institutionid=5688&courseid=52395730

BRITISH COUNCIL GREAT BRITAIN Study UK English Search

Home Why study in the UK? Plan your studies Scholarships and funding More

Home > University of Reading > MSc Agricultural Economics

University of Reading MSc Agricultural Economics

Visit website Enquire

Return to search results

**Key Information**

Tuition Fees (GBP£): 22,350 Per year  
 Start date: 30 September 2024  
 Study mode: Full Time  
 Duration: 12 months

Enquire

**Course details**

Level of study: Postgraduate

**Summary**

**Overview**

Develop your understanding of economic concepts and theories that promote world agricultural development with our MSc Agriculture Economics master's degree. With an ever-increasing world population and growing pressure on the world's finite resources, the analytical skills of agricultural economists are more relevant than ever.

**Learning**

You will have the option to specialise in a development pathway that will provide you with an area of expertise within agricultural development economics. You can also choose from a diverse range of modules that aim to give you the knowledge and skills you need to hang on.

Angalia "Entry requirements" ili ujue kama unakidhi kuomba. Sehemu niliyoikozesha kwa rangi ya bluu inanihitaji niwe na IELTS score ya 6.5, au TOEFL ya 88 kama unavoona:

search-study-uk.britishcouncil.org/course/details.html?institutionid=5688&courseid=52395730

BRITISH COUNCIL GREAT BRITAIN Study UK English Search

Home Why study in the UK? Plan your studies Scholarships and funding More

**Entry criteria**

Normally a good undergraduate honours degree (2:1 or above), or equivalent from a university outside the UK. Applicants who have relevant career experience are also welcome to apply. You will need an intermediate knowledge of microeconomics and quantitative methods, however, strong applicants with little or no training in economics may be admitted, provided you attend a pre-sessional economics course. **IELTS: 6.5 overall with no element less than 5.5 (or equivalent). TOEFL (iBT): 88.**


Visit website Enquire

**Similar course options**


Up

Sio chuo hiki tu, takriban vyuo vyote vya Uingereza huweka hitajio la IELTS au TOEFL kwa waombaji wan je ya Uingereza (International students). Hata hivyo unaweza ukaomba na ukapata udahili katika vyuo hivi bila ya kuwa na IELTS au TOEFL. Mfano mimi sina IELTS wala TOEFL lakini nimedahiliwa na naendelea na masomo hapa University of Reading. Unachotakiwa kufanya ni aidha kutumia barua ya uthibitisho kuwa umesoma undergraduate kwa kiingereza (English proficiency letter) mfano kama niliouweka katika kurasa inayofuata. Au unaweza kutumia cheti chako cha O level chenye grade ya B ya Kiingereza Au watumie email chuo husika ukiwaelezea kuwa unamudu kiingereza kwa ufasaha hivyo wakuondoshee hitajio la IELTS au TOEFL au wakupe mbadala wa mitihani hiyo miwili. **Kwa upande wangu,** wakati nafanya maombi haya sikuwa najua kuwa wanaweza wakanidahili bila ya kuwa na

IELTS au TOEFL (na ndio wengi tunaamini hivi kwa vyuo vya Ulaya hutoboi bila IELTS au TOEFL) Hata hivyo nilijizima data nikaomba hivyo hivyo. Kwa hiyo nilingia katika tovuti ya chuo husika kisha nikafanya maombi kama kawaida. Nilingia tovuti ya [University of Reading](https://www.universityofreading.ac.uk/) na nikafanya maombi ya kada ya "MSc Agricultural Economics". Sehemu ya IELTS niliweka barua ya uthibitisho wa kusoma shahada ya awali kwa kiingereza niliyopewa na chuo kama mnavoiona hapa chini:



Chuo kilinijibu maombi yangu kama ifuatavyo:



Mahali pa kuzingatia ni hapa:

for the MSc in Agricultural Economics (full time)

**Your offer is conditional upon satisfying the following conditions by the Programme Start Date:**

Achieve a minimum score of 6.5 in IELTS (Academic) (with no element scoring below 5.5) or the equivalent score in one of our other acceptable English qualifications. A list of ones we accept with scores is available at [www.rdg.ac.uk/ad-EnglishTests.aspx](http://www.rdg.ac.uk/ad-EnglishTests.aspx)


Submit two satisfactory references. Please ensure that your references are sent directly from your referees professional or institutional email account.

Please note that we cannot accept the document you have provided as confirmation of your English language proficiency. A list of acceptable proficiency tests is available at [www.rdg.ac.uk/ad-EnglishTests.aspx](http://www.rdg.ac.uk/ad-EnglishTests.aspx)

Attached to this letter you will find the **Terms and Conditions for**

Kwamba wamenipa offer (Conditional offer) kusoma MSc Agricultural Economics lakini kwa sharti kuwa niwapelekee IELTS na recommendation 2 kutoka kwa referees wawili. Kumbuka hio statement "Please note that we cannot accept the document you have provided as confirmation of your English language proficiency" inakataa ile barua niliyopewa chuoni kama nilivyoiweka hapo juu.

Lakini wametuma kiunganishi hapo kinachosema "A list of ones we accept with scores is available at [www.rdg.ac.uk/ad-EnglishTests.aspx](http://www.rdg.ac.uk/ad-EnglishTests.aspx)" Ukifungua kiungo hiki utagundua kuwa grade B ya English language katika cheti cha O level kinapokelewa na chuo hiki (na vyuo vyengine) kama kithibitisho kuwa unaweza kumudu kuwasilianana kwa kiingereza. Angalia picha hapo chini,



The screenshot shows a web browser window displaying the University of Reading Admissions page. The URL in the address bar is [reading.ac.uk/admissions/acceptable-english-language-proficiency-tests](http://reading.ac.uk/admissions/acceptable-english-language-proficiency-tests). The page has a green header with the University of Reading logo and 'Admissions' text. Navigation links for 'Staff', 'Student', and 'A-Z lists' are present. A search bar is on the right. The main content area is titled 'Acceptable English Language tests' and contains the following text:

This page contains a guide to the only acceptable English language tests that can be used to meet a condition of offer (normally made in terms of IELTS scores) made by the University of Reading.

If the test you are intending to take is not listed, please contact the Admissions Team for advice using the details on the right.

Please note that this information may change as rules on acceptability change so please do keep checking back.

**Tests acceptable for entry onto a Pre-session English programme**


Test	Test name

On the right side, there is a 'Contact Admissions' box with the following information:

- International Foundation Programme**  
ifpadmissions@reading.ac.uk
- Undergraduate Programmes(full- and part-time)**  
ugadmissions@reading.ac.uk
- Postgraduate (taught and research) Programmes**  
pgadmissions@reading.ac.uk
- PGCE Programmes**  
teachertraining@reading.ac.uk

Cambridge	IELTS (Academic) for UKVI SELT
Cambridge	IELTS Online
CBSE/ ICSE/ State boards	Indian Standard XII English (English Core/ English Elective/ Functional English)
CSE	National Examinations Council of Tanzania Certificate of Secondary Education (or Secondary Leaving Certificate)
Duolingo	Duolingo English Note: Not acceptable for Speech & Language Therapy programmes
ETS	TOEFL: Internet (our DI code is 0769)
ETS	TOEFL at home iBT

Baada ya kuwatumia cheti cha O level na recommendation 2 kutoka kwa referees wangu, walinipa Unconditional offer (barua ya kudahiliwa bila ya sharti lolote) kama mnavoona hapa chini:



Na hivi ndivyo nilivyoweza kupata “unconditional offer” kutoka University of Reading.


**ZINGATIA:** Inakuhitaji kuchangamka, kuwa makini na kusoma kila unachoelekezwa, laiti nisingelisoma maelekezo husika nisingeweza kubaini jambo hili. Tafadhali uliza au fanya mawasiliano na wahusika kama timu ya udahili (admission team) iwapo utapata changamoto yoyote. Muhimu ni kujua namna ya kuwasiliana hasa kwa kutumia email.

## KUHUSU DEPOSIT.

Vyuo vingi baada ya kukupa offer (aidha conditional au unconditional) watakwambia kuwa unahitajika kulipa "DEPOSIT" ili kuwahakikishia kuwa offer yako utaikubali. Mara nyingi huwa ni paund 2,000 (takriban mil6.5 za kitanzania) kwa vyuo vingi (japo hutofautiana). Hutakiwi kulipa hii, unachotakiwa kufanya ni kuwapa taarifa kuwa upo katika mchakato wa kuomba Commonwealth scholarship hivyo wasubiri mpaka majibu ya ufadhili yakitoka. Waandikie email nzuri ukijielezea takwa lako.

## NAMNA YA KUANDIKA EMAIL (Professional email)

Andika kichwa cha habari (heading) katika "Subject" na maelezo yako katika "Compose", Anza na salamu, jitambulishe kisha elezea hitajio lako, mfano:





## VIPINDI VYA GOOGLE MEETING

Kutakuwa na vipindi vya maswali na majibu kuhusu commonwealth master's scholarship vitakavyofanyika kupitia google meet. Vipindi hivi vitahudhuriwa na baadhi ya wanufaika wa Commonwealth Scholarships ambao aidha watawasilisha mada au watajibu maswali ya waombaji. Unaweza kujiunga kupitia kiunganishi kilichopo katika jedwali hapo chini siku ikifika au unaweza kutumia kiunganishi kifuatacho cha Google Calender ambacho kitaziweka tarehe hizi pamoja kiunganishi cha google meet katika Kalenda yako na itakurahisishia kukukumbusha siku ikifika: <https://calendar.app.google/rtvgcjojlzcxxyqab6>  
Vipindi hivyo vitafanyika kama ilivo katika jedwali hapa chini:

<b>SIKU NA MUDA</b>	<b>KIUGANISHI CHA GOOGLE MEET</b>
<b>JUMAMOSI 14/09/2024</b> <b>SAA 10;30-11:30 jioni</b>	<a href="https://meet.google.com/crz-kaxd-ddy?authuser=0&amp;hs=122">https://meet.google.com/crz-kaxd-ddy?authuser=0&amp;hs=122</a>
<b>JUMAMOSI 21/09/2024</b> <b>SAA 10;30-11:30 jioni</b>	<a href="https://meet.google.com/crz-kaxd-ddy?authuser=0&amp;hs=122">https://meet.google.com/crz-kaxd-ddy?authuser=0&amp;hs=122</a>
<b>JUMAMOSI 28/09/2024</b> <b>SAA 10;30-11:30 jioni</b>	<a href="https://meet.google.com/crz-kaxd-ddy?authuser=0&amp;hs=122">https://meet.google.com/crz-kaxd-ddy?authuser=0&amp;hs=122</a>
<b>JUMAMOSI 05/10/2024</b> <b>SAA 10;30-11:30 jioni</b>	<a href="https://meet.google.com/crz-kaxd-ddy?authuser=0&amp;hs=122">https://meet.google.com/crz-kaxd-ddy?authuser=0&amp;hs=122</a>
<b>JUMAMOSI 12/10/2024</b> <b>SAA 10;30-11:30 jioni</b>	<a href="https://meet.google.com/crz-kaxd-ddy?authuser=0&amp;hs=122">https://meet.google.com/crz-kaxd-ddy?authuser=0&amp;hs=122</a>

Saa ni za Kiswahili na ni kwa masaa ya Tanzania. Tunashauriwa kujiunga dakika 10 kabla kwa kuwa kipindi kitaanza ndani ya muda tajwa lakini pia kujihakikishia nafasi kwa kuwa Google meeting iliyotumika hapo ni ya free version hivyo ina ukomo wa watu 100 tu. Iwapo wahudhuriaji watakuwa wengi tutamia livestream ya Youtube ili waliokosa waweze kujiunga.



## KWA NINI NIMEANDIKA MUONGOZO HUU?

Miongoni mwa yaliyonipelekea kuandaa muongozo huu ni pamoja na kuyaenzi maono ya viongozi waasisi wa Taifa na misingi ya SUZA (SUZA Core values) kama nilivyonukuu hapa chini:

NUKUU KUTOKA KWA VIONGOZI WAASISI WA TAIFA LA TANZANIA.



"Hakuna mtu anayetutaka kuwapenda wengine zaidi ya tunavyojipenda wenyewe, lakini kwa baadhi yetu tuliobahatika kupata elimu nzuri tunawajibika kuboresha ustawi wa jamii tunamoishi, ni sehemu ya kujipenda sisi wenyewe" Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere.



"Jambo moja ni wajibu wetu tukwambieni vijana. Jambo lenyewe ni hili, kwamba msidhani kuwa hii Serekali yenu itaendeshwa na watu wasiokuwa nyinyi. Ni heshima kubwa kila mwananchi leo aliye kijana, aliyesoma mpaka Darasa la nane au kuendelea mbele au asiyesoma nia iwe moja ya kujenga nchi..." Hayati Sheikh Abeid Amani Karume.



MIONGONI MWA NUKUU 3 KUTOKA KWENYE MISINGI MIKUU YA SUZA (SUZA Core Values)

- + Kupenda na kuchochea mabadiliko katika jamii (Embrace and drive changes)
- + Kuwa na mtazamo chanya kwa jamii (Good intentions)
- + Kuwa mzalendo kwa taifa. (Patriotism)

**Lengo kuu la kuandaa muongozo huu pamoja na miongozo mengine ya ufadhili, ni kuongeza uelewa kwa watanzania wenzangu juu ya fursa hizi za ufadhili. Pia kuongeza idadi ya watanzania wanaoomba na wanaochaguliwa katika fadhili hizi.**

**Pamoja na kuungana na juhudi za watanzania wenzangu waliopata nafasi hizi na wanaowasaidia wengine kupata nafasi hizi.**

## MIONGOZO MENGINE

Usikose Kufatilia Miongozo Mingine Kama Vile:

Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Commonwealth PhD Scholarships  
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Commowealth Shared Scholarships  
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Chevening  
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Serekali ya China (CSC type A &B)  
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Serekali ya Indonesia (KNB)  
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa India (ICCR)  
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa Erasmus Mundus  
Muongozo wa uombaji wa ufadhili wa DAAD scholarships

Na miongozo mengine kadri nitakavyoweza kuiandaa kulingana na uzoefu niliopata wakati naomba fadhili mbalimbali (Fadhili zote tajwa hapo juu niliziomba isipokuwa ICCR). Tafadhali tumia kiunganishi hiki ([https://drive.google.com/drive/folders/1TfyG9g-YRh1K77ODKIZqd1dNeVXQYBsM?usp=drive\\_link](https://drive.google.com/drive/folders/1TfyG9g-YRh1K77ODKIZqd1dNeVXQYBsM?usp=drive_link)) ili kuweza kuangalia miongozo mengine ya fadhili mbalimbali pindi iwapo tayari.

MPAKA KUFIKIA HAPA SINA ZAIDI YA KUKUTAKIA KILA LA KHERI NA MAFANIKIO MEMA.  
NATUMAI MUONGOZO HUU UTAKUFAA NA UTAWAFAA WENGINE.  
AHSANTE.

Iwapo utakuwa na maswali na utahitaji msaada tafadhali wasiliana nami kupitia:

[mahfoudh.mahfoudh@suza.ac.tz](mailto:mahfoudh.mahfoudh@suza.ac.tz) au 0787483930 (Whatsap only)

Au jiunge na kundi sogozi la Whatssap la "Scholarship for Tanzanians" kupitia kiuongo hiki:

<https://chat.whatsapp.com/F1L7kVdNALO7NTcUUZbnXP>

Ni mimi ninayejali mafanikio yako:

Mahfoudh Mohamed Mahfoudh

Msimamizi wa semina (Tutorial Assistant-Agribusiness)

Department of Agricultural Extension and Community Development

School of Agriculture

State University of Zanzibar.

**Ruhusa ya kusambaza kwa kila anayehitaji imetolewa**

©2024